**East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature**

OPEN ACCESS

*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya

Volume-7 | Issue-11 | Nov- 2024 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2024.v07i11.002

**Review Article**

# Upekee wa Usawiri wa Wahusika Katika Fasihi Bulibuli ya Kiswahili: Mfano Kutoka *Utenzi wa Shufaka*

Rosemary Njeri Burundi[1*], Dkt. Allan Mugambi[1], Dkt. Timothy Kinoti M'Ngaruthi[1]

[1]Chuo Kikuu cha Tharaka, Kenya

**Article History**
**Received:** 21.09.2024
**Accepted:** 26.10.2024
**Published**: 06.11.2024

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Makala hii inanuia kutathmini upekee wa usawiri wa wahusika katika ushairi bulibuli wa Kiswahii kwa kurejelea. *Utenzi wa Shufaka.* Utenzi huu ulitungwa zamani na Hassan bin Aluwi na una jumla ya beti 285. Kwa mujibu wa Njozi (1999), utenzi huu haujavutia utafiti wa kitaaluma tangu ulipochapishwa mara ya kwanza katika jarida la Kijerumani - *Zeitschriftfur Africanishen* 1887. Mswada wa pekee wa utenzi huu ulipatikana katika maktaba ya German Oriental Society mjini Halle ambapo ulihifadhiwa baada ya kupelekwa hapo na Ludwig Krapf mwaka wa 1854. Knappert (1967) aliutafsiri katika lugha ya Kiingereza katika jarida la *Swahili V. 37(2)*. Katika utangulizi wa kazi yake, Knappert aliubainisha kama utenzi muhimu kwa sababu mbili; ni wa kale, na ni mmoja kati ya sanaa sifika ya fasihi ya Kiswahili. Moja kati ya kazi iliyoshughulikia utenzi huu ni ya Njozi (1999). Amebainisha kuwa utenzi huu ni mfano wa kazi ya fasihi iliyotungwa kwa usanii wa hali ya juu ili kuibua hisi za hadhira ambayo ni sehemu muhimu sana ya utendaji wa tendi. Kipengele cha wahusika ni muhimu katika kutunga kazi yoyote ya kifasihi. Kinashirikishwa na vipengele vingine vya kifani ili kuwezesha mtunzi kutoa maudhui au ujumbe wake. Watunzi wa kazi ya kifasihi huwasawiri wahusika kisanaa ili waweze kuwakilisha watu tofautitofauti katika maisha halisi ya jamii wanayotungia. Watunzi pia hutumia mbinu mbalimbali kusawiri upekee wa sifa na hulka zinazowapambanua wahusika ili kuweza kukidhi mahitaji ya kuwa vipasa sauti vya ujumbe wanaowasilisha. Makala hii inalenga kufafanua upekee wa sifa na tabia za wahusika waliotumiwa katika *Utenzi wa Shufaka*. Pia tunakusudia kubainisha kuwa, ushairi hasa tenzi huwa na wahusika waliojengwa kikamilifu kwa kutumia mbinu mbalimbali za kimtindo na za lugha. Huu ni utafiti wa maktabani. Makala hii imegawika katika sehemu tatu; sehemu ya kwanza ni utangulizi; unaotoa muhtasari kuhusu *Utenzi wa Shufaka*, sehemu ya pili inaangazia dhana ya wahusika katika fasihi na sehemu ya tatu wahusika katika tenzi kwa jumla na sehemu ya nne sifa na hulka za kipekee za wahusika waliotumiwa na mtunzi ili kuwasilsha ujumbe wake.

**Keywords:** Islamic literature, Oral tradition, Comparative literature, Stylistics Symbolism, Allegory.

**Copyright © 2024 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1. UTANGULIZI

Kisa katika utenzi wa *Shufaka* kinasimulia kuhusu mjadala waliokuwa nao malaika wa Mungu Jiburili na Mikaili kuhusu binadamu walioishi zamani. Walikubaliana kuwa binadamu walioishi zamani walikuwa wanahurumiana baina yao lakini wakawa na tashwishi kuhusu wale wanaoishi duniani wakati wa sasa. Mikaili alishikilia kuwa binadamu wanaoishi duniani wameipoteza imani yao katika ubeti wa+ 52 na 53. Jiburili kwa upande wake aliona kuwa msimamo wake Mikaili si wa kweli kwa kuwa bado matendo ya huruma na rehema yanaweza kushuhudiwa katika ulimwengu kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 51:

Ili kusuluhisha mabishano baina yao, Jiburili alimwomba Mikaili washuke ardhini ili kufanya uchunguzi wenyewe katika beti za 54, 55. Wanashuka ardhini katika umbo la binadamu. Mikaili kama tabibu na Jiburili kama mgonjwa mahututi anayehitaji msaada kutoka kwa wenyeji na waumini wa mji wa Medina. Walishuka katika msikiti na kuwapata waumini katika shughuli zao za ibada katika beti za 56-59. Wenyeji walipomwona mgeni anayehitaji msaada wanamwonea

***Corresponding Author:** Rosemary Njeri Burundi
Chuo Kikuu cha Tharaka, Kenya

huruma. Wako tayari kutoa dhahabu na fedha kumwezesha kupata matibabu katika beti za 66 na 67. Wanafahamu kuwa hapo mjini pao hakuna tabibu yeyote. Mgonjwa (Jiburili) anawafahamsha kuwa hana haja na mali wala fedha, alichotaka ni kupona katika ubeti wa 68. Pia aliwafahamisha kuwa anafahamu tabibu anayeweza kumtibu hapo mjini na akawapeleka hadi alipokuwa tabibu (Mikaili). Wenyeji wa mji wa Medina walipofika kwa tabibu, wako tayari kufanya lolote ili aweze kupata matibabu. Aidha wako tayari kutoa zawadi kwa tabibu ili amtibu mgonjwa (Jiburili) kama anavyoeleza mtunzi katika beti za 81-83. Tabibu (Mikaili) aliwaleza kuwa mgonjwa angepata nafuu kwa kupakwa damu ya kijana mwanamume ambaye ni mtoto wa saba wa mama, ambaye amesalia baada ya nduguze sita kufariki katika utoto wao katika beti za 84-88.

Maelezo ya tabibu yalilanda Kasimu mtoto wa tajiri mmoja wa hapo mjini katika ubeti 89. Ili kutimiza ahadi zao kwa tabibu, wenyeji wa mji wa Medina walienda na kumpasha habari baba yake Kasimu kwamba itabidi mtoto wake wa pekee atolewe kafara ili damu yake itumike kumtibu mgonjwa. Babake Kasimu alikubali mtoto wake atolewe kafara katika ubeti wa 144 na kuwaelekeza wenyeji wa mji wa Medina kwa mkewe katika ubeti wa 117, ili naye atoe uamuzi wake. Mtunzi anatueleza kuwa Mamake Kasimu alikubali mtoto wake wa pekee atolewe kafara ili mgeni ambaye amepatikana hapo mjini apate nafuu katika ubeti wa 64. Kama babake, Mamake Kasimu aliwaelekeza kwa Kasimu mwenyewe ili atoe rai yake kwa kuwa hakuna kiumbe ambaye ni hai angependa kutenganishwa na roho kama inavyobainika katika ubeti wa 138. Kasimu, kama wazazi wake alimwonea huruma mgonjwa na kukubali roho yake itolewa ili kuyanusuru maisha ya mgonjwa ambaye amepatikana katika maskani yao.

Kasimu aliwajibu katika ubeti wa 155 kuwa amekubali yote na aliyachukulia hayo kama mapenzi ya Mola. Baada ya familia yote kuridhia matakwa ya tabibu (Mikaili), masharti yalitolewa kuwa baba ndiye atamchinja mtoto wake katika ubeti wa 173. Kwa uchungu alitekeleza mauaji kama alivyoagizwa. Mji wote ulighubikwa na wingu la simanzi. Baada ya kushudia baba akimuua mtoto wake ili kunusuru maisha ya mtu ambaye hafahamu asili yake. Hakuna aliyezungumza na mwingine. Katika hali hiyo, mtunzi anatueleza kwamba mgonjwa na tabibu walitoweka machoni pa umati uliokuwepo na kupaa mbinguni. Umati uliachwa katika hali ya mshangao. Hawakuwa na la kufanya isipokuwa kuomboleza na kutayarisha mazishi kama anavyoeleza mtunzi katika beti za 197-208. Kitendo hicho kikawa ishara kuwa kuu kutoka kwa Manani

Baadaye malaika Jiburili na Mikaili walishuka mara ya pili katika msikiti ambapo wenyeji wanaomboleza na kutayarisha kumzika Kasimu kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 222. Wakati huu, wanajitokeza kama binadamu wasafiri wenye njaa na kiu wanaohitaji chakula haraka ili kuepuka mauti kama inavyobainika katika ubeti wa 225 na 226. Jiburili anaomba kuonyeshwa mtu ambaye ni mwingi wa ukarimu ambaye angemsaidia. Kisadfa aliyejitokeza ni babake Kasimu aliyekuwa amehuzunika kwa kifo cha mtoto wake. Licha ya kuwa na huzuni aliwashughulikia kwa upesi wenye njaa. Aliagiza mkewe kwenda nyumbani na kuwatayarishia chakula. Katika mazungumzo yao, malaika ambao ni binadamu wenye njaa na kiu, walimtambua mwenye ukarimu kama yule tajiri aliyetoa mwanawe kafara ili kunusuru mgonjwa katika ubeti wa 244. Malaika Jiburili anaomba Mola amfufue Kasimu, pamoja na nduguze sita waliokuwa wamefariki hapo awali katika ubeti wa 258.

Familia ya Kasimu pamoja na wenyeji wa mji wa Medina walifurahi na kusherehekea ushindi huu au fadhila hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Baada ya tukio hili, malaika wanapaa tena mbinguni ambako wanakubaliana kuwa binadamu walio duniani bado walikuwa na shufaka, ukarimu na imani kuu. Pia, waliafikiana na kutabiri kuwa wale binadamu watakaokuja baadaye wataasi Mola, watakosa imani na watakuwa na tamaa ya mali. Aidha, walitabiri kuwa binadamu watakuwa wenye kujitakia makuu kama inavyobainika katika ubeti wa 269. Utabiri huu kulingana na Jiburili umeshatimia katika ulimwengu wa sasa.

**2. Maoni ya Watalaamu Kuhusu Dhana ya Wahusika**

Wahusika ni kipengele cha kifani ambacho hakijitokezi waziwazi katika mashairi kama ilivyo katika tanzu nyingine za fasihi. Mashairi mengi ya kawaida hayategemei wahusika binadamu ili kuwasilisha ujumbe na kwa sababu hiyo pamekuwa na dhana kuwa mashairi hayana wahusika. Kulingana na King'ei na Kemoli (2001), watunzi wa mashairi huwatumia wahusika kwa nadra sana. Kauli ambayo inatatiza kwa kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na si lazima wawe watu Utafiti uliofanywa na Samba (2018) na M'Ngaruthi (2017, 2019) ulibainisha kuwa ubunifu wa watunzi wa mashairi huwawezesha kusawiri vihusika na wahusika wa aina mbalimbali ili kuakisi sifa na tabia za binadamu katika jamii wanayotungia.

Chimerah na Njogu (1999), wanaeleza kuwa wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaobuniwa na msanii kutokana na mazingira yake ili kuwakilisha binadamu wa kawaida. Kwa hivyo tunapochunguza sifa na upekee wa wahusika, tunazingatia ukweli kuwa wamepewa sifa tofauti tofauti kutegemea dhamira zinazokusudiwa kuwasilishwa. Wahusika ni nguzo muhimu kwa kuwa ndio dira ya matukio yote yanayopatikana katika kazi husika. Wataalamu hawa wanaendelea kueleza kuwa mashairi ya masimulizi huwa na wahusika ambao hufungamanishwa na usimulizi na huwa nguzo kuu ya kisa na ujumbe unaowasilishwa.

Msokile (1993) ameeleza kuwa wahusika ni vitu, wanyama au viumbe katika kazi ya fasihi. Wazo hili

limeshadidiwa na Wamitila (2003). Wahusika hushabihiana na binadamu kwa kuwa kazi za fasihi huandikwa kwa ajili ya binadamu. Kwa hivyo, mashairi yanakuwa na wahusika wanyama, wadudu na vitu vingine au vihusika ambavyo hupewa uhai na sifa za kibinadamu na kutumiwa na watunzi kama nyenzo ya kutolea ujumbe.

Wamitila (2002, 2008) anawaeleza wahusika kama vielelezo vya watu wanaopatikana katika ulimwengu halisi ingawa wataalamu wa fasihi wanakubaliana kuwa si lazima sifa zote za wahusika katika kazi za fasihi zifungamane moja kwa moja na wanadamu. Hawa ni viumbe wa kisanaa ambao ni nyenzo tu ya kutolea ujumbe. Wanabuniwa kutokana na mazingira ya msanii kuakisi masuala teule ya kijamii ambayo msanii anakusudia kuyabainisha. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijiografia, kitamaduni, kihistoria, kisiasa au kiuchumi. Si watu halisi bali matokeo ya ubunifu wa msanii

**3. Aina za Wahusika katika Tenzi**

Tenzi za kale ambazo zinarejelewa kama fasihi bulibuli ndizo za mwanzo katika fasihi ya Kiswahili. Gibbe (1994) alipendekeza istilahi 'Fasihi Bulibuli' kurejelea kazi za sanaa ya maandishi ya Kiswahili ya karne ya kumi na nane ambazo utunzi wake kimaudhui na kifani ulikuwa wa kiwango cha juu ukilinganishwa na kazi zilizoandikwa baadaye. Baadhi ya tenzi hizi ni kama *Utenzi wa Tambuka* ulliotungwa na Mwengo Athuman (1728), *Utenzi wa Hamziyya* uliotungwa na Muhammad bin Said Al-Busiri na kufasiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Sharif *Aidarus (1748), Utendi wa Ras al- Ghuli,* uliotungwa na Mgeni bin Faqihi, *Utenzi wa Al-inkisafi uliotungwa na Sayyid Abdalla bin Nassir (*1810-1820*)* na *Utenzi wa Mwana Kupona* uliotungwa na Mwana Kupona (1858). Kazi hizi na nyingine nyingi zimeendelea kuwa maarufu katika fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo, *Utenzi wa Shufaka* unaozingatiwa katika utafiti huu ni kati ya fasihi bulibuli ya Kiswahili.

Wahusika wanaojitokeza katika tenzi ni wa aina mbalimbali kutegemea maadili na desturi zinazothaminiwa katika utamaduni wa jamii zilizoibua tenzi husika. Tenzi nyingi zina wahusika wakuu ambao ni mashujaa. Wamitila (2008) anamrejelea mhusika mkuu katika utenzi kama mhusika wa kiepiki. Anaendelea kueleza kuwa mhusika wa namna hii ana sifa ambazo zinamweka kwenye ngazi ya juu anapolinganishwa na wahusika wa kawaida wanaopatikana katika kazi nyingi za fasihi. Sifa hizi zinahusiana na maisha, wasifu, uwezo na matendo yake. Usawiri wa mashujaa katika tenzi umekiuka uhalisi wa watu tunaowafahamu katika jamii. Japo baadhi yao wana nafsi mahususi, tabia na hulka bainifu za watu wa kawaida katika shughuli zao za kila siku, wameonyeshwa wakiwa na uajabu ulio nje ya uwezo wa binadamu wa kawaida. Wana nguvu za kimwili, kiakili, kivita na za kisihiri. Wanatenda matendo ambayo binadamu wa kawaida hawezi. Kwa mfano Mikidadi na Mayasa ni mashujaa wa *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* ambao weledi wao katika vita umekosa ukawaida. Sifa na nguvu zao za kupambana zimewafanya waonekane si watu wa kawaida. Aidha Fumo Liyongo katika *Utendi wa Fumo Liyogo* ana kimo na nguvu ya kubeba shehena inayoweza kujaza nyuma nzima peke yake miongoni mwa mambo mengine ya ajabu aliyoyatenda.

Zaidi ya mashujaa, katika tenzi kuna wahusika wapinzani au mahasimu ambao huwa vikwazo katika maisha ya mashujaa katika kuafikia jaala zao. Kwa mfano Sultani wa mji wa Pate katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni mpinzani aliyejaribu juu chini kumwangamiza. Aidha katika tenzi tuna wahusika wengine ambao huwasaidia mashujaa au wapinzani wao. Wanaweza kuwa jamaa, marafiki au watumishi wao. Pia katika tenzi kuna wahusika ambao si binadamu au viumbe wa ajabu kama vile malaika, mungu, jini au wanyama ambao mashujaa hukumbana nao katika maisha yao na inabidi wawashinde. Kwa mfano katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, Mikidadi alikumbana na jini lililotishia kumwangamiza. Alifaulu kuliangamiza kwa silaha ya imani yake kwa kukiri nguvu za Maulana.

Katika kutamatisha sehemu. ni vyema kueleza kuwa aina za wahusika katika tenzi hutegemea maudhui na dhamira za watunzi. Si tenzi zote zinasimulia matukio ya ushujaa na mashujaa wa kihistoria, kidini au kitamaduni. Baadhi ya tenzi zinatoa mafunzo kuhusu maisha na mienendo bora wa waumini kutokana na mafundisho ya Kurani kama *Al Inkishafi na Utenzi wa Mwana Kupona*. Kwa hivyo, uteuzi wa wahusika unaathiriwa *na* maudhui, dhamira na mazingira ya utunzi miongoni mwa mambo mengine.

**4.0 Upekee wa Usawiri wa Wahusika katika Utenzi wa Shufaka**

*Utenzi wa Shufaka* unaweza kuainishwa kama utenzi wa kidini kutokana na ujumbe au maudhui yaliyopewa kipaumbele. Kwa msingi huu wahusika wanaopatikana katika utenzi huu wanaweza kuainishwa katika makundi mawili: wahusika wa kihalisi ambao ni binadamu wanaopatikana katika hali halisi. Hawa ni Babake Kasimu, Mamake, Kasimu na wenyeji wa Mji wa Medina. Kwa upande mwingine tuna malaika wa Mungu Mikaili na Jiburili na Mungu ambao si binadamu. Hawa ni wahusika wa ajabuajabu ambao wanapotangamana na binadamu wana sura za binadamu wa kawaida lakini pia wana sifa za kiungu.

**4.1 Babake Kasimu**

Babake Kasimu katika utenzi huu, ni mmoja wa waumini na wenyeji na mji wa Medina. Mtunzi hajampa jina, anamrejelea tu kama baba wa Kasimu. Chacha (1992), ameeleza kuwa matendo ya binadamu huathiriwa na imani walionayo kwa Mwenyezi Mungu. Huyu ni mmoja wa waumini na matendo yake yamembainisha kama muumini wa ngazi ya juu. Katika ubeti wa 98, anarejelewa kama" mwingi wa dini". Pia mcha Mungu katika ubeti wa 108, kuonyesha kuwa imani yake thabiti

katika dini ilitambulika kwa wengine. Maneno yake katika beti za 109-117 yanadhihirisha imani yake kuu. Alipopashwa ujumbe kuwa mtoto wake wa kipekee alihitajika achinjwe kama mbuzi ili damu yake ipakwe mgeni mgonjwa ili apone, alikubali na kusema kuwa hayo ni mapenzi ya Jalali na kwamba ili mtu afe, Mungu ndiye huamuru. Aliwasisitizia waumini wenzake kuwa, hata angekuwa na watoto elfu moja katika ubeti wa 110, na iwe wote wanahitajika kutolewa kafara, kama ilivyo kwa huyu mmoja, bado angeridhia kwa imani kuwa hayo ni mapenzi ya Mungu.

Babake Kasimu amesawiriwa kama tajiri aliyekuwa na mali nyingi katika ubeti wa 89. Alimiliki fedha, dhahabu, watumwa na watumishi kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 100- 102.Yuko tayari kutoa mali yake ili kumrehemu mgeni mgonjwa miongoni mwao hata ile ya siri aliyokuwa amejihifadhia kama anavyoeleza katika beti zifuatazo:

100 Kwanza ndugu sikilizani,
tawambiya ya sirrini
nina zikwi sabuini
nyumbani nimuwekea

101 Nina zidi akithari
fedha na dinaari
fungu la Mola Jabbari
lanipeshalo kutowa

Babake Kasimu katika beti hizi, amesawiriwa kama mkweli ambaye anawafichulia hata yale ambayo hawafahamu. Aliwaeleza kuwa alikuwa na elfu mia saba ya mali aliyoweka kwa ajili ya fungu la Mola bila kuogopa kwamba wangempora. Alikuwa tayari kutoa hizo na nyingine zaidi ili kumpokeza mgonjwa apate nafuu. Anachothamini katika maisha si mali wala watoto bali ni kupata thawabu kutoka kwa Mungu kwa kutenda mema.

Aidha amesawiriwa kama mnyenyekevu na mwenye mkabala mwema na wenyeji wa mji wa Medina. Umati ulipofika nyumbani kwake na kumweleza habari za kuhuzunisha kwamba mtoto wake wa pekee alihitajika kutolewa kafara ili kumrehemu mgeni mgonjwa, aliwakaribisha ndani katika ubeti wa 98 na kuwaomba kwa unyenyekevu wamweleze kilichokuwa kimewapeleka pale. Maneno yake katika ubeti wa 94 ni kama yafuatayo:

Enyi wana wa Mangani
kwangu muesiwa nini
tafadhali naambiani
haja mliyo kujia

Baba Kasimu pia, ni jasiri ambaye haogopi chochote alichoamini ni matakwa ya Mwenyezi Mungu. Alipoagizwa na tabibu kumchinja mtoto wake mwenyewe japo kwa uchungu alitekeleza alivyoagizwa katika ubeti wa 172, kwa imani kwamba Mungu atamrehemu. Kwa utiifu alitekeleza masharti ya tabibu huku machozi yanamtiririka kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 173-174). Sifa hii ya utiifu ilimwezesha kufaulu mtihani wa malaika wa Mungu bila kujua.

Katika beti za 168 na 227, Baba Kasimu amesawiriwa kama mtu mkarimu. Licha ya kuwa na huzuni wakati wa mazishi ya mtoto wake, alimwagiza mkewe kwenda nyumbani na kuwatengenezea chakula wasafiri wenye njaa waliofika msikitini na kuomba kupewa chakula na maji. Hakuzuiwa na huzuni ya kumpoteza mtoto wa pekee katika hali ya ajabu, kuwakirimia wageni walioingia msikitini na kutaka kusaidiwa bila kujali kinachoendelea. Wageni hawa ni Malaika wa Mungu katika sura za wenye njaa na kiu.

Baba Kasimu amesawiriwa kama mwenye huzuni. Mtunzi anaeleza jinsi alilia hadi akashindwa kufungua macho yote mawili. Machozi yaliyomtoka yanamithilishwa na maji ya mafuriko au gharika katika ubeti wa 125. Kama mzazi ana uchungu wa kumpoteza mtoto wa pekee ambaye amebaki baada ya wengine sita kufariki.

Aidha, Baba Kasimu ni mwenye hekima. Katika ubeti wa 89 na 289, anarejelewa kama 'mtu mume mwerevu' na 'mwenye akili nyingi' mtawalia. Hekima yake pamoja na imani inamwongoza kutenda matendo ambayo yalimwezesha kupita mitihani ya kiimani aliyopitia. Bila kujua aliamua kuwakirimia wenye njaa licha ya kuwa ana huzuni ya kuzika mtoto wake. Chakula kinapoletwa, wasafiri wenye njaa wanataka aketi nao ili ukarimu wake utimie kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 238: Alipowajibu kuwa ana huzuni na bado hajamzika mtoto wake katika beti za 240 na 241, Jiburili alimsaili zaidi katika ubeti 242 na 243, na kupata kujua mtoto aliyerejelewa alikuwa Kasimu. Jiburili aliomba mtoto huyu afufuliwe pamoja na wengine sita waliokuwa wamefariki awali. Kwa hivyo, Babake Kasimu alifaulu kupita mitihani yote ya Malaika wa Mungu kupitia matendo yakeya kiimani. Mtunzi hakumpa jina maalumu kwa sababu alitaka msomaji kuzingatia majukumu ya kijamii. Anawakilisha umuhimu wa mzazi na muumini katika jamii.

### 4.2 Mamake Kasimu

Kama mumewe, Mamake Kasimu amesawiriwa kama muumini aliye na imani kuwa yote yanayowapata ni matakwa ya Mwenyezi Mungu. Amesawiriwa kama mwenye mlahaka mwema na watu. Mtunzi katika ubeti wa 125, anamrejelea kama 'mtu mke mlimwengu' kumaanisha mwanamke anayejua kuishi na watu ulimwenguni.

Alipotembelewa na kundi la watu kwake aliwakaribisha kwa wema. Mamake Kasimu yu tayari kuwatendea yote yaliyowafanya kwenda kwake kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 121. Mtunzi katika ubeti wa 125, anaeleza:

Mutu muke mulimwengu,
kuuza; iwile tangu,
muyile takani kwangu,

ambalo lawajibiya.

'Mamake Kasimu anataka kujua kile kimewapeleka kwake na kuwaahidi kukitekeleza katika beti za 126-127. Kama mumewe alipoelezewa kuwa walitaka mtoto wa pekee auawe ili damu yake itumike kama dawa ya kutibia mgeni mgonjwa, alikubali na kusema maneno yale yale yaliyotamkwa na mumewe. Katika ubeti wa 132, mtunzi anasema:

Laula kwamba aindi
alifati auladi
bi Hak Allah wadudi
hawangawiye fidiya

Mamake Kasimu alisema kuwa, hata kama angekuwa na wana elfu moja na kwamba Mungu anataka wawe fidia kwa mgonjwa angewatoa wote. Hii ni imani ya hali ya juu hasa kwa mama mzazi ambaye ana huyu mtoto mmoja tu baada ya wengine kufariki. Mamake Kasimu ni mtiifu. Mumewe alipomwagiza kwenda nyumbani na kutayarishia wageni wasafiri wenye njaa na kiu chakula alifanya hivyo bila ajizi kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 233. Aliondoka haraka na kuwaacha waombolezaji wakiendelea na shughuli za kutayarisha maziko ya mtoto wake wa pekee. Japo ana huzuni baada ya kupoteza watoto sita anaenda nyumbani kutayarishia wenye njaa chakula ili kuokoa maisha yao. Ni mtumishi wa Mungu kama inavyobainika katika ubeti wa 119 anayeamini kuwa, kumtimizia mja haja zake ni kumtumikia Mungu.

**4.3 Kasimu**

Kasimu alikuwa ni mtoto wa pekee wa wazazi wake ambaye amebaki baada ya wengine sita kufariki. Katika kisa hiki, yeye ni mwathiriwa. Tabibu ameeleza kuwa damu yake ndiyo ingemtibia mgonjwa mahututi ambaye amepatikana katika mji wao. Maelezo ya tabibu yanamlanda yeye katika beti za 83-87. Baba na mamake wamekubali mtoto wao atolewe kafara ili kumtibu mgonjwa huyo kwa imani kuwa watapata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungukatika beti za 109 na 134) Mama yake baada ya kuridhia yote anataka umati uliomtembelea uende hadi kwake Kasim ili wapate jawabu lake katika ubeti wa 135. Alitaka mtoto ajiamulie yeye mwenyewe kwa kuwa suala la kifo ni zito kwa binadamu. Kukubali kufa ili kuiokoa roho ya mtu mwingine si jambo rahisi.

Kasimu amesawiriwa kama mtu mwenye shufaka au huruma nyingi. Baada ya kuelezwa yaliyohitajika katika ubeti wa 150-151, aliwajibu katika ubeti wa 155 kama ifuatavyo:

Nitikiye moyo wangu
nitegemeye Muungu
mupendale ndugu zangu,
nimezipita awaa

Amekubali kufa ili kuokoa roho ya mgeni mgonjwa katika mji wao. Ana imani kuwa haya ndiyo Mola amemtakia katika ubeti wa 156, anasema:

Haya si ya mugeni
wala si yangu yakini
ni Khatwi, yakwe Manani
aliyo nikutubiya

Kauli ya Kasimu kuwa roho yake kuhitajika ili kuokoa roho ya mwingine ni mpango wa Manani ni dhihirisho la imani ya hali ya juu. Kama wazazi wake amekubali kuwa fidia ya kuokoa maisha ya mtu mwingine kwa imani kuwa hayo ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Imani yake ni kwamba yale Mola amemtakia hana budi kuyakubali. Imani yake kuu ilimpa ujasiri wa kukubali kifo kilichotekelezwa na babake mzazi ili kuokoa roho ya mtu mwingine ambaye hamfahamu. Kitendo cha Kasimu kinaweza kulinganishwa na cha Yesu katika imani ya Wakristo. Japo katika muktadha wa kisa hiki, Kasimu alitakiwa kuridhia na wazazi wake, kinyume na Yesu ambaye alijitoa kufa kwa ajili ya wokovu wa binadamu kutimiza mpango wa Mungu.

Kasimu ni mwenye huzuni. Alipoona babake akitokwa na machozi alihuzunika na kulia zaidi katika ubeti wa 186 na kumwomba babake amfunge kwa kamba miguuni na mikononi katika beti za 188 na 189, ili atakapokuwa anakata roho asitapatape.

Kasimu amesawiriwa kama jagina ambaye amejitolea kufa licha ya kufahamu uchungu atakaopitia na ukweli kuwa mwanadamu harudi baada ya kutengana na roho yake. Ako tayari kukabili kifo bila woga. Kwa ujasiri alimwambia babake na waliokuwa wamemzingira wanyamaze na kuwa hatamani kuliliwa katika ubeti wa 187:

Wanenile khayiweza
bwana wakwe kimweleza
sikyo kiliyo nyamaza
sitamani kuliliwa

Kupita kwa Baba Kasimu, Mama na Kasimu mtunzi amebainisha shufaka ya hali ya juu kwa binadamu. Hawajui asili wala fasili ya mgonjwa anayehitaji kuopushwa na mauti. Hii ni familia yenye imani kuwa wanaishi kutekeleza matakwa ya Mungu.

**4.4 Mtume Mohammed (SAW)**

Mhusika Mtume Mohammed (SAW) katika utenzi huu, amejitokeza katika masimulizi ya mtunzi. Japo hajitokezi wazi kama mshiriki wa vitendo, athari yake kwa wahusika wakuu inaonekana kama nguzo kuu ya imani yao. Sifa za Mtume Mohammed (SAW) zimesawiriwa katika beti za 18-45. Katika ubeti wa 18 mtunzi amembainisha kama mitume mpendwa. Alipendwa zaidi na Mwenyezi Mungu.miongoni mwa mitume wengine.

Aidha, Mtume Mohammed (SAW) amesawiriwa kama muungwana kutoka Uarabuni katika ubeti wa 18. Muungwana ni mtu mwenye adabu njema na tabia zilizokubalika katika jamii (TUKI, 2004).

Katika historia ya Mtume Mohammed (SAW), imefahamika kuwa alizaliwa katika familia ya Kiarabu iliyokuwa maarufu na iliyoheshimika sana.

Mtume Mohammad (SAW) amepewa sifa ya kuwa mtakatifu. Ni mtu ambaye hana kasoro wala fedheha katika ubeti wa 18. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu alimchagua na kumpa ujumbe ili auwasilishe kwa binadamu. Ni 'Tumwa Musutafa' katika ubeti wa 30. kumaanisha aliyetakaswa na Mungu. Mtume Mohammed (SAW) ni mwaminifu. Mtu mwaminifu hutenda kama anavyoagizwa. Katika ubeti wa 20, mtunzi anatueleza kuwa 'Suyu Nabii amini' yaani ni nabii mwaminifu na Mwenyezi Mungu alipompa nguzo tano za Uislamu, alifahamu kuwa angewezakuzihifadhi, kuziishi kwa uaminifu, pamoja na kuzifafanua kwa binadamu.

Mtume Mohammed (SAW) ni mwenye akili pevu. Amesawiriwa kama mwenye hekima iliyomwezesha kuhifadhi Kurani akilini kabla ya kuandikwa katika ubeti wa 24. Alipewa Sala, Saumu na Zaka na kuzihifadhi katika akili yake. Alizikariri vyema. Katika ubeti wa 23 mtunzi anatueleza:

Huyu ndye maarufu,
si kauli adhaafu,
na katika musuhafu,
aliko tubeinia

Sifa ya busara pia imeelezwa katika ubeti wa 30 kama 'mjuzi wa maarifa na mulevu wa kutambua'. Aidha ni mwombezi. Amesawiriwa kama mtume wa kuwaombea wafuasi wake ili kuwaepusha kutokana na maafa. Katika ubeti wa 24, mtunzi ameeleza:

Ndiye mupawa swalati,
na Swaumu na zakati,
na kushufai ummati,
siku ya nyota na njaa

Mtunzi katika katika ubeti huu ameelezewa kuwa Mohammed (SAW), alipewa Sala zote ili awe akiwaombea wafuasi wake (umma) siku ya kiu (nyota) na njaa kumaaanisha wakati wa haja. Vile vile ni mkweli katika ubeti wa 19. Mtunzi anaeleza kuwa ndiye mtume hakika na wa kwanza 'kubuathiwa' kumaanisha kuwa ndiye mtume aliyepewa mamlaka zaidi na Mola. Alipanda ngazi hadi akaonana ana kwa ana na Mwenyezi Mungu katika ubeti wa 21, na akapewa Kurani aliyohifadhani moyoni mwake. Akapeleka ujumbe alioingizwa kwa binadamu na Mwenyezi Mungu.

Mtume Mohammed (SAW) ni nuru. Katika ubeti wa 21, amesawiriwa kama jua lenye nuru na kuwa aliumbwa kutokana na nuru. Mtunzi anatueleza katika ubeti wa 25:

Ndiye Tumwa muddathini,
shamusi li- Anuwari,
Mukhulukuwa kwa Nuri,
isiyo kuzizimia

Katika ubeti huu Mtume Mohammed anarejelewa kama jua linalotoa nuru isiyoweza kuzimika. Kwa wafuasi wake ni mwangaza wa kuwamulikia njia anayotaka Mwenyezi Mungu. Alipewa wahyi na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuwaongoza binadamu kwa njia iliyo nyoofu. Pia Mtume Mohammed (SAW) amerejelewa kama mchungaji wa mifugo. Kwa wafuasi wake anawaongoza katika sala ili waongoke. Kati ya mitume wote ndiye amepewa mamlaka zaidi kama inavyoelezewa katika ubeti wa 19:

Ndiye mwingi mamlaka,
mbele za Mola Rabbuka,
ndiye Mutume hakika
na kwanza kubuathiwa.

Katika utenzi huu, huruma ndiyo sifa kuu inayosisitizwa na kubainishwa kupita kwa wahusika wakuu. Wafuasi wa Mtume Mohammadi{SAW) pia wameiga matendo ya kiongozi wao. Malaika wa Mungu katika utenzi huu wamethibitisha kuwa bado katika dunia kuna waumini wa kweli wenye huruma. Wamethibitisha hili kupitia kwa Baba Kasimu, Mamake na Kasimu mwenyewe Mtume Mohammed (S.A.W) ni mwenye shufaka. Hii ndiyo sifa kuu aliyopewa katika. ubeti wa 27, mtunzi anatueleza:

Swalla Allahu aloika
mwana mzaliwa Makka
mwinyi moyo wa Shufaka
na huruma za pamoja.

Aidha Mtume Mohammad (SAW) ni mwenye mamlaka. Mtunzi ameonyesha kuwa alipewa mamlaka zaidi ya mitume wote. Katika ubeti wa 22, mtunzi ameeleza kuwa ndiye aliyekuwa karibu na Mungu kuliko wengine. Uhusiano wake na Mola umefananishwa na ule wa 'waya na uta wake'. Pia ameumbiwa peponi na masabaha wake kama Ali Abubakari Omani, Athumani na Haidari.

Mtume Mohammed (S.A.W) ni mzazi mwema. Katika utenzi huu amesawiriwa kama mtu au binadamu wa kawaida. Ni babake Kasimu na bikira Mwanafatuma katika ubeti wa 29. Watoto wake pia ni wenye nuru kama taa.

Katika kutamatisha sifa za Mtume Mohammed (S.A.W), mtunzi ameonyesha jinsi yeye alikuwa Kurani kwa kuwa alitekeleza kwa matendo na mafunzo yote kwa uaminifu. Waumini wanatarajiwa kuiga mfano wake.

**4.5 Mwenyezi Mungu (S.W.T)**

Katika *Utenzi wa Shufaka* mhusika Mungu (S.W.T) amejitokeza kupitia kwa masimulizi ya mtunzi na ushuhuda wa waumini. Mungu amesawirira kama mwenye rehema kuu kwa kuwa anawarehemu waumini na hata makafiri bila kubagua katika ubeti wa 16. Sifa hii pia inajitokeza katika ubeti 97 ambapo wenyeji wa Mji wa Medina wanaenda kwa babake Kasimu kufuatia maelezo ya tabibu (Mikaili). Walipofika kwake, walimwomba amrehemu mgonjwa miongoni mwao ili

naye azidishiwe rehema na Mungu mwenye rehema. Mtunzi anaeleza:

Twapenda wamurehemu,
moyowe usitakimu,
naye Muungu Halimu,
rehema takuzidiya,

Katika ubeti huu, rehema ya Mungu ni zaidi yake binadamu. Babake Kasimu anaombwa amrehemu mgonjwa kwa kutoa mtoto wake auawe na damu yake itumike kama tiba. Babake Kasimu alipoambiwa haya alijawa na furaha na kuwajibu kuwa atawatimizia yote katika ubeti wa 79. Sifa hii pia imejitokeza katika beti za 124, 154 na 284.

Mwenyezi Mungu (S.W.T) amesawiriwa kama hakimu. Katika ubeti wa 246, anarejelewa kama 'Kadhi li-hajati' yaani hakimu mwenye uwezo. Yote atakayoamua hutimia. Hii ndiyo sababu Jiburili alimuomba ili amfufue Kasimu aliyekuwa amejitolea kufa ili kumrehemu mgonjwa. Mungu alimfufua kama alivyoombwa na Jiburili pamoja na nduguze sita waliokuwa wamekufa.

Mungu hujibu maombi. Jiburili katika ubeti wa 246 anamuomba Mungu anayejibu maombi akiwa na hakika kwamba maombi yake yatajibiwa. Anasema katika mshororo wa pili: 'Ya Mujibu daawati' yaani anayejibu maombi. Maombi ya Jiburili yalitimia kwa kuwa Kasimu na nduguze sita waliokuwa wamefariki walifufuka. Kitendo hiki kinadhihirisha imani ya waumini kuwa Mungu atawafufua ili waingie peponi.

Mungu (S.W.T) ni mwenye huruma na mpole. Sifa hizi zinajitokeza katika beti za 248 na 249. Kwa mfano katika ubeti wa 248 Jiburili anasema;

Nakuliwu li Latifu
kudurayo maarufu
wa baba nuni na kafu
watakalo lakuwiya

Katika ubeti huu Jiburili anaeleza sifa za Mungu kuwa huruma yake (kudura) ni kuu. Katika ubeti wa 249, mtunzi amerejelea sura ya mwisho ya Kurani tukufu ili kubainisha huruma ya Mungu. Sura ya Yaasini inaeleza jinsi Mungu anavyowajali wanadamu na kuwaonyesha upendo wake kupitia rehema, msamaha na ukarimu wake usio kikomo.

Mungu (S.W.T) ni mwenye kuumba na kuumbua. Jiburili baada ya kuomba na kumtukuza Mungu aliita Kasimu aliyekuwa mfu akisubiri kuwekwa kaburini ajiunge naye katika kula chakula alichokuwa ameandaliwa katika ubeti 253. Kasimu alisimama kwa idhini ya Manani. Aliyekuwa mfu amefufuliwa na kuumbwa upya na Mungu muumba na kuwa hai, pamoja na ndugu zake sita waliokuwa wamekufa Sifa ya Mwenyezi Mungu kama muumba wa viumbe vyote inaonyesha nguvu na uwezo wake wa kipekee wa kuleta uhai. Ana uwezo wa kufanya mabadiliko, kuendeleza, na kudumisha kila kiumbe kulingana na mpango wake. Kasimu na ndugu zake walikuwa wafu lakini wakawa hai tena.

Aidha Mungu amesawiriwa kama mwokozi. Katika maombi ya Mikaili na Jiburili kuombea walimwengu walimrejelea Mungu kama mwokozi ambaye ana uwezo wa kuokoa binadamu ambao wanaendelea kupotoshwa na shetani, adui wa Manani. Katika ubeti wa 274, mtunzi anatueleza:

Allahuma Muwawazi
twokowa ndiwe Mwokozi
utufunge kwa majazi
yako tumwaye shufaa

Katika ubeti huu malaika wa Mungu wanamwomba aokoe binadamu na awafunge na thawabu kwa kuwajaza shufaka yake. Sifa hii ya inasisitiza kuwa Mungu huwa tayari kuingilia kati kwa niaba ya mwanadamu ili kuwaokoa kutokana na matatizo yao, kuwaelekeza kwenye njia sahihi zitakazowaongoza kuelekea wokovu na furaha ya milele.

Mungu ni msamehevu. Amepewa sifa ya kuwasamehe wenye dhambi na kuwaepushia waumini balaa inayoweza kuwapeleka jehanamu katika ubeti wa 283 na 284. Mtunzi katika kutamatisha utunzi wake anaomba kama katika ubeti wa 282:

Tujaaliye Ghaffari
na mauti ya nadhari
dhambi ziwe maghafuni
tusionane na baa

Anamwomba Mungu mwenye kusamehe awasamehe wenye dhambi. Mungu yuko tayari kusamehe na kusaidia mwanadamu kuanza upya iwapo atamgeukia kwa toba na kutaka msamaha. Sifa hii ya Mungu kama msamehevu inaonyesha jinsi upendo na rehema zake hazina kikomo, na hutoa faraja kwa wote wanaotafuta msamaha.

Aidha Mungu ni mtukufu. Mungu hutukuzwa wakati wote. Hili linaonekana na kudhihirika baada ya tajiri kumuua mtoto wake ili kumrehemu mgonjwa. Baada ya malaika kutoweka pindi tu baada ya Baba kumuua mtoto, yeye na waumini walioshuhudia haya walimtukuza Mungu. Mtunzi anatueleza katika ubeti wa 198:

Wakahimidi Mannani
na Mutu meweamini
wakamba hili ni Shani
shani lakwe Mwinyi kuwa

Babake Kasimu na waumini wa nji wa Medina waishuhudia kitendo cha mgonjwa na tabibu ambao ni Malaika wa Mungu kupaa juu kama ishara kutoka kwa Mungu mwenye nguvu. Walimtukuza na kumwabudu Mwenyezi Mungu kabla ya kuanza kutayarisha kumzika Kasimu. Sifa ambazo zinaonyesha upekee wa Mwenyezi Mungu (SWT) katika utenzi huu, zimebainishwa kupitia

kwa usimulizi wa mtunzi na mazungumzo kati wahusika na ushuhuda wa waumini.

**4.6 Jiburili na Mikaili**

Katika *Utenzi wa Shufaka* na tenzi nyingine katika fasihi ya Kiswahili ambazo zina maudhui ya kidini, wahusika Jiburili na Mikaili wametumiwa. Katika utamaduni wa Kiislamu inaaminiwa kuwa Malaika ni watumishi waaminifu wa Allah. Pia, ni wengi na kila mmoja ana jukumu maalumu. Ni viumbe wa akili na wanaishi mbinguni. Kazi zao ni pamoja na kumtii Mwenyezi Mungu, kupeleka ujumbe kwa manabii au binadamu, na kutekeleza majukumu mengine kulingana na maelekezo ya Mungu.Wanapotumwa, huchukua sura na maumbile tofauti tofauti. Kwa mfano, Abraham na Nabii Loti walikuwa wanaume.

Mikaili na Jiburili ni wahusika ambao wanaupa utenzi huu sifa ya kiajabu. Wanaweza kujigeuza kuwa katika maumbo ya binadamu katika beti za 42-52, wanajadiliana kuhusu binadamu wanaoishi ardhini. Walipokosa kuafikiana kuhusu matendo ya binadamu wanaoishi ardhini waliamua kushuka ili wafanye upelelezi wenyewe. Walishuka ardhni katika umbo la binadamu katika ubeti wa 53. Mikaili akiwa tabibu, na Jiburili kama mgonjwa mahututi kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 55.

Katika kutangamana na binadamu Jiburili na Mikaili waligundua kuwa, binadamu walioishi ardhini wanatenda matendo yaliyodhihirisha huruma na ukarimu kinyume na alivyofikiria Mikaili katika ubeti wa 52-53. Mikaili alikuwa amedai kwamba matendo ya ukarimu na huruma yalikuwa ya zamani. Baba Kasimu, Mamake na Kasimu walidhihirisha huruma ya kiwango cha juu pale walipokubali Kasimu afe ili kuokoa roho ya mgonjwa aliyepatikana miongoni mwao.

Kati ya Malaika hawa, Jiburili amesawiriwa kama muamuzi. Aliamua kuwa washuke hadi ardhini waliko binadamu ili wajionee wenyewe katika ubeti wa 54 na 58, ukweli wa mambo. Pia walipofika mbinguni baada ya uchunguzi wao alikuwa wa kwanza kumuuliza Mikaili iwapo amepata jawabu kuhusu suala walilokuwa wamebishana juu yake. Katika ubeti wa 212, mtunzi anayadondoa maneno ya Jiburili kwa Mikaili.

Kamuwuza filihali
ewa ndugu Mikayili
uiwene-yi Suwali
naliyo kushindaniya

Jiburili anataka kujua kutoka kwa Mikaili kama amejionea kuwa watu wana huruma. Mikaili alikubaliana na Jiburili na akamuuliza amwombe Jalali amfufue kijana (Kasimu) kwa kuwa maombi yake yangejibiwa katika ubeti wa 216:

Muombe Mola Wahabu,
ahuyike muarabu,
duayo musutajabu,
ainda Allahi Taa.

Katika ubeti huu Jiburili amebainishwa kama malaika aliye na ukuruba zaidi na Mola. Dua yake kwa Jalali ingejibiwa kama anavyosema Mikaili. Sifa hii ya Jiburili kama malaika mkuu aliyeheshimika zaidi inabainika pia, katika beti za 218 na 219 ambapo Mikaili anamhimiza kufanya upesi kuzungumza na Mungu. Katika ubeti wa 219 Mikaili anasema:

Na wenda wa maarufu,
mbele za Mola sufufu,
muurabi Mola Latifu,
uombalo lakuwiy. a

Kwa hivyo, Jibrili ni malaika maarufu na anayeheshimika katika imani ya dini ya Kiislamu. Katika historia ya Uislamu ndiye aliyepeleka ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa Mtume Muhammad (S.A.W) kuhusu mafundisho ya dini, kanuni na maadili kupita Kurani. Ni malaika mpasha habari kwa binadamu.

Mikaili na Jiburili mara ya pili, walishuka katika mji wa Medina katika msikiti ambapo mazishi ya Kasimu yalikuwaa yakitayarishwa. Wakati huu walifika kama wasafiri wenye njaa na kiu. Walipowasili pale walitaka waambiwe ni nani kati ya hao waombolezaji mwenye sifa ya ukarimu anayeweza kuwapa chakula kama anavyoeleza mtunzi katika ubeti wa 227. Kisadfa aliyekuwa amempoteza mtoto anaagiza mkewe kwenda nyumbani upesi na kuwaandalia wasafiri (Mikaili na Jiburili) chakula kabla hawajamzika mtoto wao. Hakufahamu kuwa huu ulikuwa mtihani ambao akifaulu kuupita mambo mema yangetokea. Baadaye chakula kilipoletwa, wasafiri wenye njaa walitaka wale pamoja na aliyejitolea kuwafadhili. Kwa huzuni babake Kasimu aliwaomba kula peke yao kwa sababu hangeweza kula kabla ya kumzika mwanawe katika beti za 240-243. Hata hivyo, huzuni yake ilibadilika na kuwa furaha wakati malaika Jiburili aliomba Mwenyezi Mungu amfufue Kasimu pamoja na nduguze sita waliokuwa wamefariki awali. Malaika Jiburili na Mikaili wameleta ujumbe wa furaha kwa familia hii ya waumini waliodhihirisha huruma isiyo kifani.

**4.7 Wenyeji wa Mji wa Medina**

Katika utenzi huu wenyeji wa Mji wa Medina wamerejelewa na mtunzi kama waungwana wa Medina katika ubeti wa 69. Muungwana kwa mujibu wa Tuki (2004) ni mtu mwenye adabu na tabia zinazokubaliwa katika jamii. Waltembelewa na Malaika wa Mungu Jiburili na Mikaili katika umbo la binadamu (mgonjwa na tabibu), katika juhudi za kuchunguza matendo ya wanadamu kama kweli yalidhihirisha shufaka. Bila kufahamu azima ya Malaika, walipomwona mgonjwa mahututi amefika katika msikiti walifanya juu chini kuhakikisha kuwa amepata msaada. Tunaelezwa kuwa hali yake iliwafanya kumwendea na kumsaili zaidi katika ubeti wa 60-61. Matendo yao ya kujali maslahi ya mgeni yaliwafnya kutambuliwa kama waungwana.

Wenyeji wa mji wa Medina wako tayari kutoa fedha, dhahabu na chochote kile alichotaka katika ubeti

wa 67. Kitendo hiki kinawasawiri kama watu wakarimu. Katika mji wao hakukunwa na tabibu lakini mgonjwa alipowafahamisha kuiingia kwa mmoja hapo sokoni, waliandamana naye hadi alipokuwa. Msukumo wao ulikuwa kutaka kutenda mema kama anavyoleza mtunzi katika ubeti wa 72. Walipofika kwa tabibu, ambaye pia ni mgeni, waliagizwa kutafuta mwanamke ambaye ni mama wa watoto saba na sita kati yao wamekufa. Huyo mmoja aliyesalia ndiye alitakikana ili damu yake itumiwe kama dawa ya mgonjwa katika ubeti wa 83-87. Walitekeleza masharti yote ya tabibu na kwa babake mtoto na kumweleza kuhusu maagizo ya tabibu, kisha kwa mama na mwisho mwathiriwa mwenyewe ambaye alikubali kufa ili kuiokoa roho ya mtu mwingine.

Katika kisa hiki Wenyeji wa mji wa Medina, wamesawiriwa kama watu wemaWanaongozwa na nia yao ya kutumikia wale walio na shida. Imani yao ni kuwa kwa kufanya hayo watapata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mgonjwa ambaye ni malaika wa Mungu alikuwa mgeni kwao lakini walionyesha mapenzi na utu kwa kutaka kumsaidia kutokana na hali mbaya ya afya iliomkumba.

## 5. HITIMISHO

Katika utafiti huu tumedhihirisha kuwa tenzi huwa na wahusika waliosawiriwa kwa njia ya kipekee inayowawezesha watunzi kuwasilisha ujumbe wao. Katika utenzi huu wahuska waliosawiriwa wamedhihirisha msimamo imara wa kiimani kuwa yote yanayotokea katika maisha huwa katika mpango wa Mulana. Kasimu alirithia kufa ili kuokoa maisha ya mtu mwingine kwa imani kuwa ni mapenzi yake mola. Wazazi wa Kasimu walikubali mtoto wao wa pekee awe sadaka ya kumnusuru mgeni kwa imani kuwa watapata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Matendo yao yanaonyesha misimamo hatari ya inani katika dini inayopelekea muumini kujitoa mhanga ili kuokoa maisha

## MAREJELEO


- Chacha, N. C. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi.* University of Dar es Salaam.
- Chimerah, R., & Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Gibbe, A. G. (1994). *Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia.* Tasnifu ya Uzamifu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi.
- Knappert, J. (1967). *Utenzi wa Shufaka, The Story of Compassion* katika Swahili, 37(2), 133-137.
- M'Ngaruthi, T. K. (2019). Umbuji wa wahusika Katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka kwa Diwani ya Jicho la ndani katika *East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature (*vol.2 Toleo la 6) uk.296-300
- M'Ngaruthi, T. K. (2007). *Usawiri wa Wahusika katika Dafina ya Umalenga na Jicho la Ndani.* Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta
- Njozi, H. M. (1999). Critical Artistry in Utenzi wa Shufaka katika. *Nordic Journal of African Studies,* 8(1), 117-129. imepakuliwa kutoka https://www. researchgate. net>2422
- Samba, M. R. (2018). *Uhusika katika Mashairi ya Kiswahili: Malenga wa Vumba, Kichomi* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Maseno.
- TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Kanifu* (Toleo la pili). Oxford University Press.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Focus Publishers Ltd.
- Wamitila. K. W. (2006). *Kamusi ya Ushairi*. Vide-Muwa.
- Wamitila. K. W (2008). Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fashi. Vide-Muwa Publishers Ltd.


**Cite This Article:** Rosemary Njeri Burundi, Dkt. Allan Mugambi, Dkt. Timothy Kinoti M'Ngaruthi (2024). Upekee wa Usawiri wa Wahusika Katika Fasihi Bulibuli ya Kiswahili: Mfano Kutoka *Utenzi wa Shufaka*. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 7*(11), 355-363.